**Learning By Ear 2011 Biashara – Kuanzisha Biashara**
**Kipindi Cha 3: "Kutoka katika fikra hadi mpango kamili"**
AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel, Adrian Kriesch
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

**Characters**

Msimulizi

Daniel Huba (mwanamume, umri wa miaka 29)

## Scene 1:

**KOSSI:** (Mwanamume, umri wa miaka 18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**MARIAM:** (Mwanamke, umri wa miaka 19)

## Scene 2:

**KOSSI:** (Mwanamume, umri wa miaka 18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**MARIAM:** (Mwanamke, umri wa miaka 19)

**LINDA:** (Mwanamke, umri wa miaka 20, dadake Kossi)

**JOHN:** (Mwanamume, umri wa miaka 21, kakake Mariam)

### Scene 3:

**KOSSI:** (Mwanamume, umri wa miaka 18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**MARIAM:** (Mwanamke, umri wa miaka 19)

**THE SECRETARY**: (Mwanamke, umri wa miaka 23)

AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel, Adrian Kriesch
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

## INTRO

### Host:

Hamjambo na karibuni kwenye kipindi kipya cha mfululizo wa vipindi vyetu vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu jinsi ya kuanzisha biashara. Marafiki watatu Mariam, Abbas na Kossi wanataka kuanzisha biashara yao binafsi. Tayari wana mawazo mengi na wanataka kuyapunguza wasalie na wazo moja. Tutaanza na ushauri wa Daniel Huba, mhadhiri wa Kituo cha Kieneo cha Ustawi wa Ujasiriamali, Chuo Kikuu cha Inoorero nchini Kenya.

### 1. Daniel Huba 40''

*Unakumbuka inakubidi kuandika wazo lako, kwa hivyo ni lazima uzingatie nani mteja wako. Katika biashara tunasema mteja ndiye mfalme. Kisha kaa chini na uamue kwa mfano, ungetaka kuuza nguo. Ikiwa ninawalenga vijana wanawake, je wanahitaji mavazi aina gani? Kwanza- mtindo wa kisasa, pili- wanazingatia sana bei kwa kuwa hawana fedha nyingi. Utakuwa ukizingatia haya kutegemea mtazamo wao. Tatu- wangependa mavazi ya kupendeza. Nne- wangependa mavazi yanayowatosha. Kwa hivi zingatia vitu ambavyo wateja wako wanavihitaji. Hali hii katika biashara hujulikana kama tathmini.*

**2. Narrator:** Sasa tusikilize jinsi wenzetu watakavyoshughulikia azma yao.

AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel, Adrian Kriesch
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

## Scene 1 : In the park

## Kossi, Abbas, Mariam

**3. SFX: outside, birds, traffic in the background**

**4. MARIAM:** (**Determined**) Jamani, tusipoteze wakati kuhusiana na jambo hili. Tuamueni mara moja

**5. KOSSI:** Kwangu mimi, tayari nimeshaamua, Mariam. Abbas, mbona unataka kuturegesha nyuma? Wewe ndiye uliyetushawishi tufikirie wazo la usanifu hapo jana, au sivyo?

**6. ABBAS:** Naam, ila nimekuwa nikiwazia…

**7. MARIAM:** Sikiza! Tumeshaamua- Tutaanzisha kampuni ya usanifu. Wewe ndiwe uliyesema tunapaswa "kufikiri urembo, kubuni urembo, na kuuza urembo"

8. **KOSSI:** (**Continues**) Na ulisema kampuni yetu itawasaidia na kuwashauri wasanifu, wanamitindo, wasanifu-ujenzi, wasanii wachoraji…

9. **MARIAM:** na ukasema kwa kuwa bara la Afrika linaingilia kwa kasi maisha ya kisasa huku miji ikiongezeka, basi huduma zetu zitawaniwa sana. Na kwamba hivi karibuni tutaongoza kwenye sekta hiyo na tutatajirika si haba …

10. **ABBAS:** Ndiyo, najua nilisema hivyo, lakini…

11. **KOSSI:** **(Interrupts him)** Sasa tunatakikana kulenga wateja tunaowakusudia kisha tuendelee na mradi wetu.

12. **MARIAM:** Lakini tayari tunajua wateja tunaowalenga – wasanifu-ujenzi wanamitindo, wasanifu …

13. **ABBAS:** Tunapaswa kulenga vijana na pia kulenga ulimwengu wa mitindo. Na kuna nyumba mpya zinazojengwa kila pahali – tunaweza kuwashauri wenyewe kuhusiana na usanifu na upambaji, na kuwa na ubia na wasanifu-ujenzi na wahudumu wa nyanja ya ujenzi.

14. **MARIAM:** (**Impressed**) Looo!, Nani kama wewe!

15. **ABBAS:** (**Softly**) Ninakuiga wewe!

16. **KOSSI:** Alaa, maneno hayo! (**Laughing**) Nadhani tunapaswa kuzungumza pia na dadangu na kaka yako, Mariam – wanaelewa mambo yalivyo kwenye ulimwengu wa mitindo.

17. **ABBAS:** Naam, wazo zuri hilo. Wanaweza kuwa washirika wetu.

18. **MARIAM:** (**Suddenly**) Mbona tusiende sasa kuzungumza nao? Udongo uwahi ungali maji! Pengine wanafanya mazoezi sasa.

19. **KOSSI:** Wanafanya – niliwaona kabla ya kuondoka nyumbani. Wanafanyia mazoezi kwenye karakana kama kawaida, wanajitahidi …

20. **SFX : Sound of chairs, door slamming, steps going off quickly. Motors starting up and moving off.**

## Scene 2: Rehearsal room at Kossi's parents

**ABBAS, MARIAM, KOSSI, JOHN, LINDA**

21. **SFX : modern instrumental music in the background**

22. **SFX : Sound of steps: high-heeled shoes / a model walking up and down, stops, goes / change of rhythm.**

23. **JOHN:** (**in a loud voice, addressing the model**) Mara nyingine… unatakikana kuzungusha visigino vyako wakati unapozungusha kiwiliwili chako…Sasa, simama, jikaushe…nenda tena, kwa kasi, zunguka…naam, kama hivyo…

24. **LINDA:** John, sijui unaonaje, lakini… nadhani kuna kitu ambacho si sawa. Anavyoshika kichwa, na jinsi anavyokwenda mbele…

25. **JOHN:** (**Imperturbable, to the model)** Simama! Vivyo hivyo – naam! Sasa, sogeza upande wa juu wa kiwiliwili chako taratibu… (**lowering his voice, to LINDA)** Ninamtazama, anapendeza si haba!

26. **LINDA:** (**In a low voice**) Taratibu, unatazamwa! Na usisahau (**in a soft but menacing voice**) – tayari wewe ni mali ya mtu!

27. **JOHN:** (**Loudly**) HAYA, HAYA, tumemaliza. Tuachie hapa.

28. **SFX : Steps moving away – a woman wearing heels.**

29. **SFX : Door squeaks**

30. **KOSSI:** Hongera!

31. **MARIAM:** (**Impressed**) Looo!

32. **JOHN:** **(Surprised)** Alaa, hamjambo, jamaa!

33. **ABBAS:** John, mambo! Sikiza bwana, tuna haja nawe. Wewe na Linda mnaweza kutusaidia kuwasiliana na watu wanaohusika na mambo ya mitindo ya mavazi? Tunataka kuanzisha kampuni ya kutoa ushauri kuhusu mambo ya usanifu na mitindo.

34. **MARIAM:** Tunataka kulenga taasisi kama hii yenu, tuwatolee huduma zetu ili wapate kutangaza vyema shughuli na hafla zao..

35. **LINDA:** Aha! Lakini mjue kwamba mna kibarua kigumu! Tayari kuna ushindani mkubwa.

36. **JOHN:** Kweli hiyo. Kampuni ya New Design inapanga kufungua tawi la bara la Afrika hapa..

37. **LINDA:** Na pia kuna Africa Design. Tayari tunashirikiana nao.

38. **MARIAM:** Lakini kwani ina maana kwamba sisi hatuwezi pia kujijengea sifa wenyewe?

39. **JOHN:** Bila shaka mnaweza – wala sina nia kuwavunja moyo. Naam, hiyo yenu ni fikra nzuri. Na tunaweza kuwasaidia. Lakini hii ni nyanja ya kipekee. Inawabidi kuzingatia hali ya mambo, hasa mahali palipo na ushindani wa kibiashara.

40. **Narrator:** **Naam, wametahadharishwa! Lakini wanaonekana kuwa na hamasa kweli kweli … hawana budi ila kuchunguza wajue ushindani ulioko, na huduma zinazotolewa. Inawabidi kutoa huduma zenye tofauti kidogo na zile zilizoko ili wapate wateja. Mtaalamu wetu Daniel Huba anaeleza:**

**41. Daniel Huba 1'**

*Kwa mfano, katika vijiji vyetu vingi kuna hizi maskani za kanda za video, ambapo watu wanaweza kununua kanda za CD na kutazama filamu. Nitajiuliza, niongezeje thamani ya kazi yangu ninapoingilia biashara ya maktaba ya kanda za video? Nitahakikisha ninawasilisha filamu zilizotolewa karibuni zaidi niwaazime wateja wakatazame. Njia moja ya kuongeza thamani ni kutambua kile wateja wangu wanachohiari zaidi. Kwa mfano, nitayasajili majina yao na kuwapelekea ujumbe mfupi wa simu kila mara ninapopata filamu mpya. Hapo ninaongeza thamani ya kazi yangu. Vipi? Kwa kuwapa wateja wangu huduma ya ziada. Kwa hivyo kuongeza thamani ya biashara yangu, si lazima nilete bidhaa au huduma mpya. Hoja muhimu*

*hapa ni jinsi ninavyoweza kufanya kwa kutumia bidhaa zilizoko, ni kitu cha ziada kwa wateja wangu. Na bila shaka hatua hiyo itawavutia zaidi wateja wangu.*

**42. Narrator:** **Marafiki zetu watatu wanahitajika kuchunguza ushindani ulioko pamoja na bidhaa au huduma zinazotolewa. Kwa hivyo Abbas, Mariam na Kossi wameamua kutembelea Africa Design – bila kujitambulisha!**

**<u>Scene 3: Paying a visit to the competition, Africa Design offices, on a busy street</u>**

**ABBAS, MARIAM, KOSSI, THE SECRETARY**

**43. ATMO: Sound of cars, beeps, passers-by talking unintelligibly**

**44. SFX : Motorbikes parking**

45. **ABBAS:** Ni hapa. Nifuateni!

**46. SFX : Sound of steps of three people, quite fast**

47. **ABBAS :** Na tujihadhari tusiropoke ovyo tutakapokuwa ndani! Kumbukeni - tumefungua kampuni ya mitindo hivi karibuni na tunatayarisha onyesho letu la kwanza la mitindo ya mavazi …

**48. SFX : Door opens and closes again.**

**49. ATMO : Office atmo**

**50. MARIAM:** (**Nicely**) Hujambo, tumekuja kutaka ushauri.

**51. KOSSI:** Sisi ni wateja watarajiwa… Kwa kweli, tuna kampuni ya mitindo ya mavazi, baadhi yetu tunahusika na urembeshaji…

**52. ABBAS:** … Tungependa kuandaa onyesho la mitindo ya mavazi, na tumependekezewa kampuni yenu.

**53. THE SECRETARY:** Karibu! Ketini. Naam…

**54. SFX: Chairs being moved**

**55. ABBAS:** Unaweza kutuonyesha baadhi ya huduma mnazotoa?

**56. THE SECRETARY:** Naam, bila shaka. Orohda hii hapa.

**57. SFX : Sound of paper, of pages being turned.**

**58. THE SECRETARY :** Tunaweza kuwashughulikia kuanzia mwanzo hadi mwisho wa onyesho lenu la mitindo ya mavazi. Tutashughulikia uendeshaji wa onyesho hilo, mahali litakapofanyika, usalama, shughuli ya kuwaalika watakaohudhuria, kupamba, na kadhalika. Lakini kwanza tunahitaji kujua mawazo mlio nayo ili tufahamu mahitaji yenu, kuhusiana na bidhaa za urembo kwa mfano …

**59. ABBAS:** Kwa hivyo mtahusika katika kila hatua?

60. **THE SECRETARY:** Naam, yote hayo kwa lengo la kushirikiana nanyi, ili muyaendeleze mawazo yenu. Nyinyi ndio wenye wazo, ndio mnaotaka kuandaa onyesho.

61. **SFX : Telephone rings**

62. **THE SECRETARY:** Subirini kidogo (**She answers**) AFRICA DESIGN, Hatujambo… Naam, naam… Bado hajafika. Ndio, mama, nitamjulisha. Bila shaka, mama. Asante, kwaheri… (**She hangs up**) Kama nilivyosema…

63. **MARIAM:** Nadhani uliyotwaambia yanatosha.

64. **THE SECRETARY:** Nataka tu kusema kwamba huwa tunajitahidi vyovyote vile kuwafaa wateja wetu kadiri ya uwezo wetu. Lakini kwanza mngezungumza na mkuu wangu. Hayupo hapa sasa hivi, lakini mkiniachia majina yenu na jinsi ya kuwasiliana nanyi…

65. **SFX : Chairs being pushed back**

66. **SFX : Sound of steps on the carpet**

67. **ABBAS** SAWA, Asante, Asante sana. Tutawasiliana kwa simu … (**They go out**) Twendeni zetu. Asante…

68. **SFX : Door opens and closes. Sound of steps.**

69. **ATMO : Noise of cars, beeps, passers-by speaking unintelligibly**

**70. MARIAM:** Hao jamaa wamepanga mambo yao vizuri sana, au siyo? Ulipokuwa ukizungumza na huyo bibi nilikuwa nikipiga jicho sehemu zote. Kila kitu safi.

**71. KOSSI:** Afisi zao pia ni nzuri.

**72. MARIAM:** Zina nafasi kubwa na hewa safi. Rangi yake pia inapendeza …

**73. ABBAS:** Itatubidi tujitahidi kuwapita. Tunatakikana kuwa tofauti, na tuwashinde kidogo tu kwa uzuri!

**74. KOSSI:** Hata hivyo wao washughulikia tu mitindo ya mavazi, ilhali sisi tuna azma ya kufanya mambo mengine pia, kama vile usanifu wa ndani

**75. ABBAS:** Naam, hiyo ni tofauti kubwa. Tunapaswa kuzingatia sana hilo!

**76. MARIAM:** Sikizeni. Twendeni nyumbani sasa. Tutachanganua akili tujue jinsi ya kuwashinda hawa jamaa. Ninaamini tunaweza!

**77. ABBAS:** Hata mimi!

**78. SFX : Motorbikes starting up, moving off.**

## OUTRO

### Host:

Ni hayo tu kwa leo katika kipindi cha Noa Bongo Jenga Maisha Yako. Usikose kipindi kijacho kuhusu kuanzisha biashara ili upate kujua mipango waliyo nayo Kossi, Mariam na Abbas. Na pia kuzingatia ushauri wa mtaalamu wetu Daniel Huba wa Chuo Kikuu cha Inoorero mjini Nairobi nchini Kenya. Iwapo unataka kukisikiliza tena kipindi hiki au vingine, tembelea wavuti yetu www.dw-World.de/lbe.Ukitaka kuwasiliana nasi, tuandikie barua-pepe kwa: www.dw.de/kiswahili

Usikose kututegea sikio katika kipindi kinachofuata! Kwaheri!

END